**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya.

*Dkt. Maureen K. Luvanda, PhD*[1]

[1] Kenya Agricultural & Livestock Research Organisation, S. L. P. 32 - 00902, Kikuyu, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-1685-2502 ; Barua pepe ya mawasiliano: maureen.luvanda@kalro.org

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*19 Aprili 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Ustawi wa Wanyama, Ukatili wa Wanyama, Maadili, Kenya, Wakulima, Wanyama..*

## IKISIRI

Hati hii imetayarishwa kushughulikia maswala ya ustawi wa mifugo nchini Kenya na kuongezeka kwa ujuzi wa wafanyikazi wa mstari wa mbele kuhusiana na swala la viwango na sheria zinazoongoza ustawi wa wanyama. Lengo kuu lilikuwa kutathmini vipengele vya utunzaji wa wanyama, matibabu na ujuzi wa ustawi wa wanyama miongoni mwa wakulima nchini Kenya. Tuligundua ya kwamba wakulima wengi hawaelewi kimsingi ustawi wa wanyama kwa kuwa wengi wao hawajapata mafunzo maalum na wengi wao hawajui sheria zilizopo kuhusu mada hiyo. Wadau wengine walitathminiwa pia kwa madhumuni ya kulinganisha na madaktari wa mifugo na kama ilivyotarajiwa walikuwa na ujuzi zaidi kuhusu ustawi wa wanyama na desturi zinazoikuza. Hata hivyo, kadhaa walionelea kwamba serikali haikuweka juhudi za kutosha katika kukuza ufahamu wa umma au hata kuhamasisha jamii dhidi ya ukatili wa wanyama. Kulingana na maelezo yaliyopatikana, hati hii iliundwa ili kutoa suluhisho ya vitendo linapohusu swala la kuongeza ustawi wa wanyama nchini Kenya. Mapendekezo haya ni pamoja na kuishinikiza serikali kuanzisha sera madhubuti dhidi ya ukatili wa wanyama, kuwahimiza maafisa wa sheria kutekeleza sheria za sasa kwa kutumia mifumo ambayo tayari iko na kuhimiza mazungumzo ya jamii na ushiriki wa moja kwa moja wa watu walio mstari wa mbele.

**APA CITATION**

Luvanda, M. K. (2022). Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 49-63. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626.

**CHICAGO CITATION**

Luvanda, Maureen K. 2022. “Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 49-63. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

**HARVARD CITATION**

Luvanda, M. K. (2022) “Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya”, *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 49-63. doi: 10.37284/jammk.5.1.626.

**IEEE CITATION**

M. K. Luvanda. “Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya”, *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 49-63, Apr. 2022.

**MLA CITATION**

Luvanda, Maureen K. “Uchambuzi wa Hali ya Ukatili wa Wanyama Katika Mashamba Nchini Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Apr. 2022, pp. 49-63, doi:10.37284/jammk.5.1.626.

## UTANGULIZI

Kulingana na Kanuni ya Afya ya Wanyama ya OIE (*Office International des Epizooties*), ustawi wa wanyama unafafanuliwa kama “hali ya kimwili na kiakili ya mnyama kuhusiana na mahali ambapo anaishi au kufa”. Hii ina maana kwamba kitu chochote kinachosumbua hali ya maisha ya mnyama kinachukuliwa kuwa unyanyasaji wa wanyama na hii inajumuisha zaidi ya vurugu. Unyanyasaji wa wanyama unajumuisha ukeketaji, usafi duni/mazingira machafu, njaa, ukosefu wa huduma za afya, kutelekezwa, usafiri usiofaa, msongamano, burudani, ukamataji na kufungwa kusiko kwa kibinadamu na kuweka mizigo mingi kupita kiasi kwenye wanyama wanaofanya kazi (Mogoa *et al.*, 2005). Aina zisizo za kawaida za unyanyasaji hutokea hasa kutokana na ukosefu wa ujuzi au unyeti kuusiana na maisha ya mnyama.

Mogoa na wenzake (2005) wanatoa ufafanuzi wazi wa ustawi wa wanyama na kuangazia uhuru tano wa kimsingi unaoandamana nayo. Wanasisitiza kwamba hali ya kimwili na kiakili ya mnyama huamua hali yake ya afya na ustawi. Hii maelezo inaambatana na ufafanuzi ulitototolewa na OIE. Zaidi ya hayo, wanaeleza kuwa utafiti wa kitaaluma katika ustawi wa wanyama umechangia uboreshaji wa sekta ya kilimo nchini Kenya kwa kuendeleza sheria za ustawi na kuathiri kuboreshwa kwa hali ya wanyama. Wanasisitiza kuwa nchini Kenya, ukatili wa wanyama hutokea kwa sababu zifuatazo 1) Ukosefu wa mafunzo ya wafanyikazi wa wanyama katika desturi za ustawi wa wanyama 2) Sera na sheria zilizopo hazitoshi na hazitekelezeki 3) Ukosefu wa huduma za ufuatiliaji ili kuhakikisha visa vya ukatili wa wanyama kuripotiwa na kuzuiliwa.

Katika nchi zinazoendelea kiuchumi kama Kenya, kuna ongezeko la soko la bidhaa za wanyama kwa sababu ya ukuaji wa miji iliyofanya kilimo kuwa biashara yenye faida kubwa sana (Thornton, 2010). Hata hivyo, ustawi wa wanyama bado hauzingatiwi kuwa kipaumbele katika maeneo haya (Kimwele *et al.*, 2011). Hili linaleta wasiwasi sana ikizingatiwa ya kuwa ni ukweli unaojulikana kuwa wanyama wanaopata matibabu ya kibinadamu wanakuwa na afya bora na huzaa zaidi. Kwa hivyo, kwa kuwa ufugaji hauzingatiwi tena kuwa shughuli inayofanywa vijijini pekee, ufugaji wa wanyama unaendelea kuongezeka kwa utaratibu katika maeneo ya mjini (Alarcon *et al.*, 2017). Kwa hivyo ni muhimu kuweka kipaumbele kwa afya, fiziolojia na hali ya maisha ya wanyama hawa. Hili sio muhimu kwa wanyama pekee yake bali kwa afya ya jumla ya ikolojia mzima ikijumuisha binadamu ambayo kwa kawaida hujulikana kama ajenda ya afya moja (*One-Health Agenda*) (Thumbi *et al.*, 2015). Afya moja hutendeka kwa kuzuia magonjwa ya zoonotiki ambayo yanaweza kuenea kama matokeo ya kupuuzwa kwa mifugo. Kimwele, Alarcon na Thumbi wote wanajadili matumizi ya wanyama kutoka kwa mtazamo wa afya moja. Kimwele anaangazia mbinu za afya moja kuhusu suala la utafiti wa majaribio, Alarcon anaangazia vivyo hivyo kutoka kwa mtazamo wa ufugaji wa mifugo mijini na Thumbi anajadili kipengele jumuishi ambacho kinajumuisha athari kwa uchumi, afya ya binadamu pamoja na afya ya wanyama.

Kuboresha matibabu na hali ya jumla ya wanyama wa shamba kutachangia katika uzalishaji bora wa bidhaa za kibiashara kama vile maziwa na mayai na hivyo kuhakikisha usalama wa chakula ndani ya mkoa unaendelea kuwa thabiti (Njisane *et al.*, 2020). Katika juhudi hizi, mbinu na desturi mbalimbali zimetumika kuboresha ustawi wa wanyama ikiwa ni pamoja na mbinu za “*conditioning*” (kuzoesha hali) na kuanzishwa kwa sheria husika zinazodai tabia za kibinadamu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

linapokuja suala la utunzaji wa wanyama (Edwards-Callaway na Calvo-Lorenzo, 2020). Aidha, ustawi wa wanyama pia umeripotiwa kuwa chombo kinachoweza kupimika kulingana na hali ya mazingira na sifa za kimwili za mnyama (Broom, 1991). Eneo la ustawi wa wanyama na maadili yake bado linachukuliwa kuwa dhana mpya kabisa inayojumuisha zaidi hali ya kisaikolojia ya mnyama katika masuala ya afya (Manning *et al.*, 2021). Ni muhimu kulipa kipaumbele eneo hili sio tu kwa faida ya mnyama bali kwa faida ya wafanyikazi wote wa mstari wa mbele wanaoingiliana na wanyama hawa kila siku na jamii yote kwa ujumla (Rioja-Lang *et al.*, 2020). Njisane, Edwards-Callaway, Calvo-Lorenzo, Broom na Manning wote wanajadili na kuangazia masuala yanayohusu ustawi wa wanyama nchini Marekani, Australia na katika jumuia za Kiafrika.

Sekta ya kilimo duniani imeonyesha mara kwa mara kwamba wanatanguliza uzalishaji wa wanyama kuliko afya (Greger, 2011). Ripoti za hivi majuzi zimeonyesha kuwa vituo vikubwa vya uzalishaji wa wanyama vinasababisha uharibifu wa afya ya wanyama na pia vinachangia kuzorota kwa afya kwa wafanyikazi wa kiwanda na wakaazi wa jamii jirani (Greger na Koneswaran, 2010). Zaidi ya hayo, usafirishaji wa mifugo kwa muda mrefu na kwa umbali mrefu umeelezwa kama fursa za kueneza magonjwa na Shirika la Chakula na Kilimo (*Food and Agriculture Organisation-FAO*) (Greger, 2007). Kwa bahati nzuri kumekuwa na kilio cha kimataifa kuhusu ustawi wa wanyama ikiwa ni pamoja na juhudi zinazofanywa na Shirika la Kulinda Wanyama Duniani (*World Animal Protection Organisation*) ambalo linajihusisha na shughuli dhidi ya kufungwa kwa karibu kwa wanyama kwa kutetea wanyama kuwa na uhuru wa kutembea na hivyo kuongeza viwango vyao vya maisha. Mnamo 1958, sheria na kanuni za kibinadamu za kuchinja ("*Humane Methods of Slaughter Act*") zilipitishwa nchini Amerika na kwa sasa zinatekelezwa na Huduma ya Usalama na Ukaguzi wa Chakula (*United States Department of Agriculture - USDA*). Sheria hizi zinataka nyumba zote za kuchinja zizingatie utunzaji wa wanyama wa kuchinjwa kwa upole na utu. Hii inaonyesha, linapohusu suala la ustawi wa wanyama katika mtazamo wa kimataifa, wasiwasi huenea hata zaidi ya shamba na kuelekea teknolojia ya kibayoteknolojia na uvumbuzi mwingine wa hali ya juu wa kiteknolojia ambao unaweza kuathiri mnyama vibaya na hata kusababisha kuongezeka kwa magonjwa ya zoonotikia.

Kutokana na ongezeko la matumizi ya nyama na bidhaa za maziwa barani Afrika, wanyama wanaofungwa huchangia pakubwa katika pato la taifa la kilimo (*Gross Dometic Product-GDP*) (Molomo na Mumba, 2014). Tangu mwaka wa 2018, Mtandao wa Afrika wa Ustawi wa Wanyama (*Africa Network for Animal Welfare-ANAW*) umeshirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*United Nations Environment Programme-UNEP*) kutetea ustawi wa wanyama katika nchi zote za Afrika kwa ushiriki wa dhati kutoka kwa jumuia ya kiraia pamoja na wadau mbalimbali. Ushirikiano huo pia umesababisha maendeleo ya Muungano wa Ustawi wa Wanyama wa Pan African (*Pan African Animal Welfare Alliance-PAAWA*) ambao unatetea ustawi wa wanyama ili kuboresha pato la kiuchumi kote Afrika. Mnamo 2017, Kenya iliandaa mkakati wa kushughulikia masuala ya ustawi wa wanyama nchini ili kuboresha hali ya kiuchumi. Hili lilifanywa kupitia shirika la Mamlaka ya Kiserikali ya Maendeleo (*Intergovernmental Authority for Development-IGAD*). Walitengeneza mipango ya utekelezaji iliyoandikwa kwa miaka ya 2017-2022. Hizi ni pamoja na "Mkakati wa Kitaifa wa Wanyama wa Kenya na Mipango ya Utekelezaji" (*Kenya National Animal Strategy & Action Plans*) na "Mkakati wa Kitaifa na Ustawi wa Wanyama wa Kenya" (*Kenya National Animal Welfare Strategy*). Utafiti wa Molomo na Mumba unaonyesha jinsi wanyama wa shambani wanavyochangia kwa kiasi kikubwa Pato la Taifa la bara zima la Afrika ambapo mamilioni ya watu wanawategemea kwa chakula na mapato. Licha ya hayo, ustawi wa wanyama bado ni suala ambalo limepuuzwa kwa kiasi kikubwa katika bara hili. Kwa hivyo wanapendekeza kwamba eneo zima linapaswa kujitahidi kuelewa haya masuala ili kuongeza tija ya wanyama na ubora wa bidhaa.

## VIFAA NA MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mbinu za ubora ambazo ni pamoja na dodoso za uchunguzi (mahojiano yenye muundo nusu) uliyofanywa kulingana na sampuli za makusudi zisizo na uwezekano. Ilijumuisha sehemu mbili ambapo moja ilizingatia idadi ya watu waliohojiwa na ya pili ilishughulikia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

ukatili/unyanyasaji wa wanyama na masuala ya ustawi wa wanyama. Uchunguzi wa kimaumbile pia ulifanywa ambao uliruhusu ufafanuzi sahihi wa upeo wa mada na kuzingatia masuala mahususi ya msingi ambayo ni muhimu zaidi. Mbinu ziliruhusu ukusanyaji wa taarifa zinazohitajika pamoja na uchunguzi wa wakulima na wafanyikazi wa mstari wa mbele katika makazi yao ya kawaida ya kila siku na taratibu pamoja na tathmini ya kina ya wafanyikazi wengine. Pia iliruhusu fursa ya kutathmini hali kulingana na maoni ya wale wenye ni wa muhimu kwenye huu msuala. Maswali yaliyoulizwa yalitokana na Itifaki za Ubora wa Ustawi (*Welfare Quality Protocols*®), uhakikisho wa shamba (*farm assurance*®) na viwango vilivyowekwa kwa sheria.

Uchunguzi na uchambuzi wa fasihi ya umma ili kupata mtazamo ya kitaaluma pia ulifanyika ili kuhakikisha uelewa wa kina wa sera za serikali na mazoea yanayozunguka ustawi wa wanyama na masuluhisho yanayowezekana. Waliolengwa walikuwa wakulima, madaktari wa mifugo na wafanyikazi walio mstari wa mbele kwa kuhudumia wanyama kama wafugaji, wachungaji, wataalam na viongozi kwenye serikali. Jumla ya mashamba 126 yalitembelewa katika mikoa iliyoonyeshwa kwenye Jedwali 1.

Ushiriki ulikuwa kwa hiari na washiriki wote walitoa kibali kabla ya kujihusisha. Isipokuwa imeelezwa vinginevyo, data yote ilishughulikiwa kwa siri.

**Jedwali 1**

*Mikoa iliyojumuishwa katika utafiti*

| | Kaunti | Kaunti-Ndogo | Wadi | Eneo Bunge |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Nairobi | Embakasi East | Utawala | Embakasi East |
| **2** | Kiambu | Kikuyu | Kinoo | Kikuyu |
| **3** | Kakamega | Lurambi | Mahiakalo | Lurambi |
| **4** | Kakamega | Navakholo | Shikorami/ Esumaiya | Navakholo |
| **5** | Kakamega | Navakholo | Ingotse Mutihu | Navakholo |
| **6** | Kakamega | Malava | South Kabras | Malava |
| **7** | Kakamega | Shinyalu | Isukha Central | Shinyalu |
| **8** | Kakamega | Shinyalu | Murhanda | Shinyalu |
| **9** | Kajiado | Kajiado West | Ewuaso Kedong | Kajiado West |
| **10** | Kajiado | Kajiado West | Magadi | Kajiado West |
| **11** | Kajiado | Kajiado West | Ewuaso Oonkidongi | Kajiado West |
| **12** | Kajiado | Kajiado Central | Dalalekutuk | Kajiado Central |
| **13** | Kajiado | Kajiado South | Entonet/Lenskim | Kajiado South |
| **14** | Vihiga | Sabatia | Busali | Sabatia |
| **15** | Vihiga | Sabatia | Chavakali | Sabatia |
| **16** | Vihiga | Sabatia | West Sabatia | Sabatia |
| **17** | Vihiga | Sabatia | North Maragoli | Sabatia |
| **18** | Vihiga | Sabatia | Wodanga | Sabatia |
| **19** | Vihiga | Vihiga | Central Maragoli | Vihiga |
| **20** | Vihiga | Emuhaya | North East Bunyore | Emuhaya |
| **21** | Vihiga | Hamisi | Tambua | Hamisi |
| **22** | Vihiga | Hamisi | Gisambai | Hamisi |
| **23** | Vihiga | Hamisi | Shiru | Hamisi |

*Maelezo*. Mikoa iliyojumuishwa katika utafiti huo ni pamoja na Kaunti 4, Kaunti Ndogo 13, Wadi 23 na Maeneo Bunge 13.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

## MJADALA

Walio kwenye mstari wa mbele ambao daima wanahudumia wanyama wanahitaji kuwa na maarifa ya kina ya mbinu bora za kutumia linapokuja suala la kuboresha ustawi wa wanyama wao. Uchunguzi wa jumla unaonyesha kwamba ustawi wa wanyama unaonekana kuwiana kwa kiasi kikubwa na hali ya juu kiuchumi, dhana ambayo tulitarajia kukatiza kwenye utafiti huu. Kwa hivyo ilikuwa muhimu kupata maoni ya wale wanaohusika moja kwa moja ili kuelewa hali halisi. Hati hii inanuia kutoa ufahamu kuhusu hali ya sasa nchini Kenya ili kueneza uanzishaji wa shughuli kama hizo kote. Pia, inaeleza kwa lugha rahisi sheria na sera mbalimbali ambazo zinahusu utunzaji, matibabu na ustawi wa wanyama.

### Tathmini ya Utaratibu wa Sera za Serikali Zinazodhibiti Ustawi wa Wanyama wa Mashambani Nchini Kenya

Ingawa machapisho ya kitaaluma kuhusu ustawi wa wanyama mahususi nchini Kenya ni kidogo, serikali ya Kenya ilitangaza katiba mpya mwaka wa 2010 ambayo ina kipengele cha kuzingatia haki za wanyama kwa kuzuia ukatili na mateso. Hii katiba inaangazia jukumu ambalo serikali inafaa kutekeleza linapokuja suala la kukuza ustawi wa wanyama ikibainisha kuwa serikali ya kitaifa inapaswa kuwalinda wanyama pori huku serikali za Kaunti zinawajibika kulinda mifugo na wanyama wa kufugwa (Katiba ya Kenya, 2010). Miaka miwili baadaye, "Sheria ya Kuzuia Ukatili kwa Wanyama" (*Prevention of Cruelty towards Animals Act*) ilirekebishwa na kuidhinishwa (Sheria nambari: SURA YA 360). Sheria hii ndio msingi wa sheria zote za ustawi wa wanyama nchini Kenya na ilipitishwa hapo awali mnamo 1953 na marekebisho mnamo 1962, 1964, 1969, 1979 na bila shaka 2012. Ilichapishwa na Baraza la Kitaifa la Kuripoti Sheria kwa idhini kutoka kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Inajumuisha sehemu nne ambapo sehemu ya kwanza inatanguliza sheria, sehemu ya pili inajadili vitendo vinavyochukuliwa kuwa makosa wakati wa kutunza wanyama, sehemu ya tatu inahusu matumizi ya wanyama kwenye utafiti wa kisayansi na sehemu ya mwisho inahusu masharti ya ziada ambayo inaweza kuwa imepuuzwa kwenye sehemu zingine. Kwa hivyo, isipokuwa sehemu ya 3, sehemu nyingine zote zina umuhimu kwa wakulima na hati hii inatoa muhtasari kwa njia rahisi ili ieleweke kwa wafanyikazi wa mstari wa mbele.

### Sheria ya Kenya Kuhusu Ustawi wa Wanyama

Kwa mujibu wa Katiba, sheria inakataza kupiga wanyama kikatili, Kusababisha maumivu kwa wanyama au aina nyingine za mateso, kuwatisha, matumizi ya wanyama wagonjwa au waliojeruhiwa au waliochoka kwa kazi, kunyima wanyama unaowatunza maji na chakula, kutowajali, kuwaweka mahali pachafu na kukataa kukidhi mahitaji yao ya kiafya kama chanjo na matibabu ya magonjwa. Makosa haya yote yanaadhibiwa chini ya sheria ya Kenya kama "hatia ya kosa la ukatili" ambayo husababisha takriban miezi 6 gerezani au faini ya chini ya shilingi elfu mia tatu au hata adhabu zote mbili. Sheria pia inakataza kupea wanyama sumu, kuwafanyia au kuruhusu wafanyiwe upasuaji haramu, kukataa kupea euthanasia kwa mnyama wakati mazingira yanadai na kuwawinda au kuwaua kinyume na sheria.

### Vizuizi vya Zaidi na Adhabu Kulingana na Sheria ya Kenya

Inaadhibishwa kisheria kushiriki kwa namna yoyote katika kitendo cha kumpiga au kumpiga chambo mnyama. Makosa hii inaweza kusababisha kifungo cha jela cha takriban miezi sita au faini ya shilingi elfu tatu au zote mbili. Kuwateka wanyama kutumia mbinu ambazo zinasababisha kujeruhiwa au kufa kwao pia ni marufuku na faini inaweza kutozwa kwa mhalifu. Zaidi ya hayo, nyenzo zinazotumiwa kutengeneza mtego au mtego wenyewe unaweza kutwaliwa na maafisa wa kutekeleza sheria. Kutelekeza mnyama akiwa katika hali mahututi kama akiwa mgonjwa au mahali pasipo salama au eneo ambapo hawezi toroka shida ikitokea au kumhusisha mnyama katika mafunzo ya kikatili kwa ajili ya maonyesho /mashindano kwa namna ambayo huleta maumivu na mateso, kuchinja kwa mnyama kwa njia ya kikatili au kumuua mnyama huku wanyama wengine wakiwa wamesimama na kuweza kuona pia huchukuliwa kuwa uhalifu. Uhalifu huu unaweza kuvutia takriban miezi tatu kwenye jela au faini ya shilingi elfu mbili au zote mbili. Aidha, vitu vyovyote vilivyotumika kufanya uhalifu huo vinaweza kutwaliwa na vyombo vya sheria.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

Filamu zinazoonyeshwa kwa umma hazipaswi kamwe kuonyesha aina yoyote ya ukatili wa wanyama. Huu uhalifu unaweza sababisha kifungo kisichozidi miezi tatu na faini ya elfu mbili au zote mbili. Kuwabeba wanyama wakati unapowauza kwa njia ambayo inakuza usumbufu wao, maumivu au aina yoyote ya mateso pia kunaadhibiwa na sheria na huvutia faini ya shilingi mia tano.

Wamiliki wa wanyama wanaoruhusu wanyama wao kudhulumiwa wanajibishwa na mahakama. Ni wajibu wa mwenye mnyama kuwalinda wanyama wake na kutofanya hivyo kutavutia adhabu au hata kuondolewa kwa wanyama kutoka kwa ulinzi wa mmiliki wake. Vilevile gharama zozote zilizotumika wakati wa kutaifisha wanyama au maagizo mengine yoyote kutoka kwa mahakama yatahamishiwa kwa mmiliki. Mmiliki aliyepatikana na hatia anaweza hata kuzuiwa kumiliki au kuishi na wanyama katika siku zijazo iwapo mahakama itashawishika kuwa kufichua wanyama kwa mhalifu kunaweza kusababisha kosa zaidi. Kukosa kuheshimu sheria kunapendekeza miezi sita jelani au faini ya shilingi elfu tatu au zote mbili.

**Sheria Nyingine**

Sheria nyingine nchini Kenya inayoshughulikia masuala ya ustawi wa wanyama ni "Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 364" ambayo inaangazia hatua zinazopaswa kuchukuliwa na mhudumu wa wanyama iwapo mnyama ataathiriwa na ugonjwa. Inabainisha kuwa mhudumu anatarajiwa kulinda wanyama wote dhidi ya magonjwa ya kuambukiza kwa hivyo analazimika kuwaweka karantini yoyote kati ya kundi lake iwapo kutashukiwa kuzuka. Ana wajibu pia ya kujulisha umma kupitia mamlaka ya karibu takwimu ya mlipuko wa ugonjwa unaoshukiwa. Ikiwa mnyama atakufa kwa sababu ya ugonjwa unaoshukiwa, utupaji unapaswa kufanywa chini ya maagizo ya afisa wa mifugo aliyehitimu.

Chini ya sheria hii pia wanasisitiza kwamba chanjo fulani kama vile Rinderpest kwa ng'ombe na mengineyo ni ya lazima na daktari wa mifugo anapaswa kushauriwa kuhusu chanjo hizi. Pia inaeleza kuwa malisho yoyote yanayotolewa kwa wanyama lazima yasiwe na magonjwa na yenye afya kwa ajili ya kuliwa na mnyama. Sheria hii pia inaeleza kuwa wanyama wanaopatikana kwa kuingizwa nchini hii kutoka nchi nyingine yoyote lazima wapimwe na kutibiwa magonjwa yoyote yanayoweza kutokea kabla ya kuruhusiwa kujiunga na wananchi kwa ujumla. Shughuli yoyote inayokiuka sheria hii itasababisha adhabu kwa takriban miezi kumi na mbili kwenye jela au faini ya shilingi elfu thelathini.

"Sheria ya Kuweka Chapa SURA 357" pia inabainisha nafasi katika mwili wa mnyama ambapo uwekaji chapa unaruhusiwa kwa madhumuni ya kusajili hisa. Inabainisha pia aina za wanyama wanaoweza kupigwa chapa kuwa ni pamoja na ng'ombe, farasi, ngamia, kondoo na mbuzi na inaelekeza mahali ambapo chuma cha chapa kinaweza kupatikana.

Sheria ya "Rabies SURA 365" imetolewa ili kupunguza visa vya ugonjwa wa kichaa cha mbwa nchini. Inatoa takwimu zilizoidhinishwa kama vile maafisa wa kutekeleza sheria, maafisa wa mifugo, maafisa wa utawala au wakaguzi haki ya kukamata mnyama anayeshukiwa kuwa na kichaa cha mbwa au hata kumuua akipatikana katika eneo la kudhibiti kichaa cha mbwa. Hii kwa ujumla iko katika kizimbani mwa wanyama kipenzio kama vile mbwa na paka badala ya mifugo. Katika kesi ya mnyama aliyeambukizwa na kichaa, mmiliki ambaye hadhibiti mnyama wake anawajibika kwa kukamatwa au adhabu kwa mujibu wa sheria. Faini inayoambatana na ukiukaji wa sheria hii ni shilingi tano kwa kila siku kutoka ripoti inapotolewa hadi siku ambayo mmiliki atamdhibiti mnyama wake.

Ikiwa mmiliki atakataa kudhibiti mnyama wake aliye na ugonjwa anaweza kufungwa jela miezi tatu au kulipa faini ya kawaida ya shilingi elfu mbili au zote mbili. Maeneo ambayo yametangazwa kuwa maeneo ya kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni pamoja na Hifadhi ya Mukogodo katika Wilaya ya Nanyuki, Tharaka, Nyambene na eneo la Malisho ya Kaskazini huko Meru, Kaunti ya Machakos - isipokuwa sehemu zilizoonyeshwa zikiwa na rangi nyekundu katika Mpango wa Mpaka Nambari 500, Mkoa wa Magharibi, Mkoa wa Nyanza, Wilaya ya Kitui katika sehemu ya ardhi ya Kamba ambayo iko hapo pamoja na Ardhi ya Serikali ya B.2 Yatta na Ardhi ya Serikali ya Mashariki. Kwa hiyo miezi tatu ya kwanza baada ya eneo kutangazwa kuwa "eneo la kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa", washikaji na wamiliki wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

wanyama wanatarajiwa kuwaweka wanyama wao kipenzi ndani ya eneo lililofungwa kama vile banda kati ya saa moja usiku na saa kumi na mbili asubuhi. Katika vipindi vingine vya wakati, wanyama wanapaswa kuwekwa kwenye kamba.

Kukosa kutii karatani iliyoidhinishwa kunaweza kusababisha kifungo cha mwezi mmoja au faini itakayoamuliwa na mahakama. Hatimaye, kuwazuia maafisa wa kutekeleza sheria wanapo kuwa katika harakati za kutekeleza majukumu yao kunasababisha adhabu ya angalau miezi sita jela au faini ya elfu tatu au zote mbili. Mahakama ya Juu inahifadhi haki ya kukamilisha maamuzi yoyote dhidi ya hukumu. Mashtaka za uwongo na hukumu zisizo za haki pia zinaweza kukata rufaa katika mahakama hii ndani ya siku saba.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Maoni ya Washiriki

Katika wakulima ambao walijihusisha na utafiti huu, asilimia 24.6 pekee ndio waliofahamu sheria za serikali zilizoangaziwa hapo mbeleni kuhusu ustawi wa wanyama huku wengi wao wakiwa wanafahamu mipango ya serikali kupambana na ujangili na Shirika la Huduma wa Wanyamapori nchini (*Kenya Wildlife Services-KWS*). 91.3% ya waliohojiwa walionyesha kuwa wangeunga mkono utekelezaji wa sheria linapokuja suala la kukuza ustawi wa wanyama na kwamba ukiukaji unapaswa kuadhibiwa na sheria; hasa katika hali ambapo wahudumu huwatesa wanyama wao.

Hata hivyo, wote walikubali kwamba utekelezaji wa sheria kuhusu unyanyasaji wa wanyama ungetekelezwa na ufanisi zaidi ikiwa kungekuwa na mafunzo ya ufahamu kwa watunza wanyama. Kilichokuwa kinawasumbua baadhi ya washiriki ni kwamba Sheria ya Kichaa cha Mbwa iliruhusu kuuawa kwa wanyama. Pia kuwa kuacha vitu vyenye sumu ndani ya mazingira ambavyo vinaweza kusababisha kifo cha mnyama huadhibiwa kwa faini ya shilingi 200 tu. Baadhi ya wafanyikazi wa mstari wa mbele walikosoa “Sheria ya Uwekaji Chapa” kwa kutotoa bunge lolote dhabiti kuhusu uwekaji chapa za wanyama kwa njia ya kibinadamu ili kushughulikia ukatili wa wanyama. Wengi wao walikuwa na maoni kwamba adhabu kali zaidi zinapaswa kuanzishwa ili kuongeza umakini linapokuja suala la kulinda wanyama dhidi ya madhara ya mazingira yanayosababishwa na mwanadamu. Ingawa sera na sheria hizi kuhusu ustawi wa wanyama zipo nchini Kenya, zinachukuliwa kuwa hazitoshi (Mogoa *et al.*, 2005) na hazitekelezwi ipasavyo katika ngazi ya chini.

### Kanuni na Imani za Kijamii Kuhusu Ukatili wa Mifugo Miongoni mwa Jamii Mbalimbali

Utamaduni na dini za Kiafrika zilionekana kuwa na jukumu kubwa katika kushawishi jinsi wakulima nchini Kenya wanavyo shughulikia wanyama wao.

### 1 Athari za Imani za Kidini kwa Ustawi wa Wanyama

Wale wanaofuata imani ya Kikristo walirejelea mfano kutoka kwenye Bibilia wa kuchunga mnyama ambaye alikuwa ameanguka shimoni wakati wa Sabato kumaanisha kwamba Imani yao inawatia moyo kuwasaidia wanyama licha ya hali zao. Wengine walirejelea kitabu cha Mwanzo ambapo Mungu alimwamuru mwanadamu kutunza viumbe vyote duniani pamoja na wanyama katika bustani ya Edeni. Wengine walisema wanatoa wanyama kama sadaka kwa kanisa hasa kwa ajili ya zaka na pia katika madhehebu yale yanayomkabidhi mtoto wa kwanza wa kiume uchungaji mara baada ya kuzaliwa. Kwa hivyo, wanyama wana jukumu kubwa katika mazoea ya kidini ambayo yanaiga agano na Mungu.

### 2. Athari za Mila za Jadi kwa Ustawi wa Wanyama

Mila za tamaduni ziliweka wanyama kipaumbele hasa miongoni mwa jamii ya Wamaasai ikionyesha kuwa wana mchango mkubwa sana katika jamii hiyo. Jamii zingine zina mila zinazoamuru wanyama kutumika kama zawadi kama vile wakati wa mazungumzo ya mahari, ishara za rambirambi wakati wa mipango ya mazishi na pia kwa madhumuni ya burudani kama vile hafla za kikanda za kupigana za mafahali. Wanyama wanachukuliwa kuwa chanzo cha utajiri na usalama na jamii kadhaa kwa hivyo pia hutumika kama ishara ya hali ya juu ya kijamii ambayo inaweza kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia hutumika kufanya mila fulani wakati wa sherehe za kutahiri na makabila tofauti yana mifumo mbali mbali isiyo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

rasmi ya kuwaadhibu wale wanaodhulumu wanyama. Wakulima katika hizi jamii wameweka viwango vya wazi vya kuhakikisha utunzaji mzuri wa wanyama wao hata wakiwa hawapo.

### Majukumu ya Kimaadili Kuhusu Ustawi wa Wanyama


Katika jamii ambazo hazina mifumo ya kitamaduni inayoendeleza ustawi wa wanyama, ilitia moyo kuona kwamba ingawa baadhi ya wahojiwa (69.84%) hawajashuhudia matukio ya ukatili kwa wanyama, asilimia 89.7 kati yao walidhibitisha kwamba ikiwa hali itatokea ambapo waliona aina yoyote ya ukatili wa wanyama wangeripoti mara moja kwa mamlaka. Mamlaka hizi ni pamoja na polisi, afisa kilimo, utawala, afisi au afisa mafugo, chifu au chifu msaidizi, ofisi au afisa wa serikali, wazee wa kijiji au mwenye shamba endapo ni hali inayohusisha mtunza mifugo aliyeajiriwa. Asilimia 30.9 walisema wangeenda mbali zaidi na kuhamasisha au kushauri pande zinazohusika kuhusu umuhimu wa ustawi wa wanyama na kutetea ukatili sifuri na haki nyingine, huku 13.5% wakisema wangesimamisha uovu huo kikamilifu hata kama mamlaka itachelewa kuingilia kati. Hii ilionyesha kwamba, kwa ujumla, watu wa mstari wa mbele wanafahamu vyema wajibu wao wa kimaadili linapokuja suala la ustawi wa wanyama na kuzuia ukatili wa wanyama.

### Maarifa ya Ustawi wa Wanyama Kati ya Washiriki

Wahojiwa hao ambao walikiri kuwa watasita kuingilia kati walithibitisha kuwa sababu kuu ni ukosefu wa mafunzo rasmi ya ustawi wa wanyama, jambo ambalo liliathiri ujasiri wao katika suala hilo ni ukosefu wa taarifa za ni wapi hasa wanaweza kuripoti suala hilo. Lakini, ni 14.3% tu walioonyesha kuwa walikuwa na ufahamu wa wasiwasi unaojitokeza kwa sasa dhidi ya ustawi wa wanyama. Waliokuwa na ujuzi walitaja baadhi ya masuala kuu waliyoyaona katika kazi zao. Walitaja kwa mfano kufanya kazi au kuwapakia kupita kiasi kwa wanyama wanaofanya kazi kama ng’ombe na punda, kutumia wanyama kwenye burudani, kuwapa wanyama dawa wasiohitaji, kuchapa au kukatakata wanyama ovyoovyo, kuwanyima wanyama chakula na maji, kuwaweka mahali pachafu, kuwafunga kwa muda mrefu, kuwalea kwenye mazingira madogo sana, kuchinja mnyama bila euthanasia, kuwahisa kusikofaa, ufugaji wa kuku kutumia mfumo wa betri, kusafirisha wanyama wakiwa kwenye vizimba, kukataa kuwatibu wanyama wanapokuwa wagonjwa na kukosa kuwalinda wanyama kutoka kwa wawindaji. 34.9% wanafahamu mila na mienendo iliyopo ambayo inakuza ustawi wa wanyama kama vile kliniki za “Tunza Punda” ambazo zinahimiza matibabu ya kibinadamu kwa punda, kutafuta huduma za mifugo wakati mnyama anaumwa au ikiwa kuna mlipuko wa magonjwa yanayojulikana au yasiyojulikana.

### Jinsia na Umri ya washiriki

Kwa mtazamo chanya, pengo la kijinsia kilionekana kuzibika katika nyanja ya ufugaji huku wakulima wa kike wakiwa 47.6% ya wahojiwa katika utafiti huu ikilinganishwa na wanaume waliopata 52.4% kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielezo cha kwanza.**




| JINSIA | n | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanaume | 66 | 52.4 |
| Wakike | 60 | 47.6 |


**Kielezo 1:** Chati ya pai inayoonyesha asilimia ya wakulima wanaume dhidi ya wanawake walioshiriki katika utafiti

Ilivutia pia kuona ya kuwa wakati wa kupanga idadi ya wakulima kulingana na umri, vijana kati ya miaka 20-29 walikuwa na uwakilishi wa kutosha ilihali wa makamo kati ya umri 40-49 ndio


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

walishiriki zaidi kama ilivyoonyeshwa kwenye **Kielezo cha pili na tatu.** Habari hii ya umri uliarifu kundi la utafiti lililojumuishwa.




**Kielezo 2**. Chati inaonyesha rika za wakulima walioshiriki katika utafiti huu kulingana na umri. Kikundi cha umri kati ya miaka 40-49 kilionekana kuhusika zaidi katika taaluma ya kilimo.




**Kielezo 3.** Chati inaonyesha wastani wa umri wa wakulima pamoja na miaka ya kazi.

## Sababu za Kiuchumi Zinazoadhiri Utunzaji wa Wanyama wa Shamba


Kwa kuwa mashirika kadhaa ya kimataifa yanatetea kubadilika kwa lishe inayotokana na mimea, tulitathmini nia ya wakulima kubadili kutoka kwa ufugaji wa wanyama hadi kilimo cha mazao pekee. Asilimia 72.2 walisema hawatabadilisha kutokana na sababu za kiuchumi na hali ya hewa. Hili lilieleweka kwa kuwa lilihusiana vyema na ukweli kwamba chini ya 5% ya wakulima waliojumuishwa katika utafiti huu walikuwa na vyanzo vingine vya mapato. Kwa hiyo, bila ufadhili wa kutosha itakuwa vigumu kuongeza maji, hali ya hewa na rutuba ya udongo. Hata hivyo, baadhi walionyesha nia ya kufanya kilimo cha mchanganyiko.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

## 1 Uchumi na Ufugaji wa Wanyama


Wakulima wengi (88.1%) walioshiriki katika utafiti huu walipendelea ufugaji wa ng'ombe ikilinganishwa na wanyama wengine kama inavyoonyeshwa katika **Kielezo 4.** Huu ulionekana kuwa uamuzi mwingine unaotokana na sababu za kiuchumi ambapo wakulima > 90% walieleza kuwa lengo lao kuu la kilimo ni kuingiza kipato na kutoa chakula kwa familia zao. Kwa hiyo, kwa kuwa kuna ongezeko la matumizi ya nyama na maziwa pamoja na uzalishaji mwingi unaopatikana kutoka kwa ng'ombe, itakuwa na maana zaidi ya kiuchumi kwa wafugaji kutegemea zaidi katika ufugaji wa ng'ombe kuliko aina yoyote ya wanyama. Lakini, mbuzi, kondoo na kuku pia walipendelewa zaidi kuliko wanyama wengine kama wanyama kipenzi wanaounda 41.3%, 33.3% na 27.8% ya wanyama, mtawaliwa. Kwa upande mwingine, punda ambao ni wanyama maarufu kwa kazi walionekana kutengeneza asilimia 20.6 pekee ikionyesha kwamba uzalishaji wa nyama ya wanyama na maziwa ulipewa kipaumbele. Zaidi ya 58.7% walionelea kuwa ustawi wa wanyama ni jambo la gharama mno huku wakulima wengi wakipendelea kuwaruhusu wanyama wao kuzurura ili kulishwa na mimea iliyopo kwenye mazingira. Ununuzi wa chakula cha mifugo na maji safi ulifanywa hasa wakati wa kiangazi na katika hali ambayo wanyama walikuwa wametengwa au karantini na wakati wa mlipuko wa magonjwa. Kama ilivyoonyeshwa katika **Kielezo 5,** wakulima wengi (93.6%) walijishughulisha na ufugaji ili kupata mapato ya kipesa. Wengine walifanya hivyo ili kupata mazao ya chakula (80.2%), kupata samadi kwa ajili ya kilimo cha ardhi (10.3%), kwa ajili ya usalama (63.6%), kama shauku (14.3%) na kwa usafiri au kazi (39.7%).




**Kielezo 4.** Grafu inaonyesha asilimia ya wakulima (mhimili-y) wanaofuga aina maalum za mifugo (mhimili-x).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626




**Kielezo 5.** Grafu inaonyesha asilimia ya wakulima (mhimili-y) na sababu zao za kujihusisha na kilimo kama taaluma (mhimili-x).

## 2 Uchumi na Afya ya Wanyama


Mambo ya kiuchumi yalionekana pia kuathiri maamuzi ya huduma za afya kama vile upatikanaji wa huduma za mifugo pamoja na chanjo. Baadhi ya wakulima walipuuza kuwachanja wanyama wao wa kipenzi kwa sababu kipaumbele kilitolewa kwa mifugo inayowaingizia mapato. Licha ya changamoto hizo, 72.2% ya waliohojiwa walikiri kutafuta huduma za kitaaluma za mifugo wakati mifugo yao ilipougua au kuhitaji chanjo. Ng'ombe walichanjwa mara kwa mara dhidi ya magonjwa ya kawaida kama vile *Foot and Mouth*, *East Coast Fever*, *Brucellosis*, *Peste des petits ruminants*, magonjwa wa ngozi kama *Lumpy*, *Black Quarter* na *Enterotoxaemia*. Wafugaji wa kuku mara kwa mara walichanja ndege wao dhidi ya ugonjwa wa *Newcastle*, *Fowl pox*, *Fowl typhoid* na *Gumboro*. Kinga dhidi ya vimelea ambavyo pia hutegemea mambo ya kiuchumi pia hufanywa hasa kila wiki kwa kutumia hatua mbalimbali za udhibiti kama vile kunyunyizia dawa za kuua vimelea na wadudu, kuokota kupe, kuchovya ng'ombe, kuimarisha vitamini na dawa za minyoo mara kwa mara. Kwa hivyo kupuuza, ambayo ni aina ya kawaida ya unyanyasaji wa wanyama, pia huimarishwa na vikwazo vya kiuchumi na hii inaweza kuathiri afya ya wanyama kwa njia kubwa.

## 3 Uchumi na Ukubwa wa Shamba

Wakulima wengi waliojumuishwa katika utafiti huu wana shamba la ukubwa chini ya ekari 150 na shamba la wastani la ekari 56 kwa kila mkulima. Hii iliamuliwa na uwezo wa kiuchumi wa mkulima binafsi. Wastani wa bajeti ya kila mwaka kwa kila shamba iliamuliwa kuwa shilingi za Kenya 170,000 kwa mwaka ambayo ni takriban shilingi za Kenya 500 kwa siku. Ingawa asilimia 97.6 kati yao wanamiliki mashamba yao binafsi, asilimia 2.4 tu yanamilikiwa na serikali au jamii, bado kulikuwa na dalili kubwa kwamba wengi wanakabiliwa na matatizo ya kiuchumi kwa sababu 33.33% yao walipata msaada wa kifedha kama ruzuku au mkopo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626




**Kielezo 7:** Grafu inayoonyesha bajeti ya kila mwaka (mhimili-y) dhidi ya wastani wa ukubwa wa shamba (mhimili-x) wa washiriki waliojumuishwa katika utafiti huu.

Usaidizi wa kifedha ulipokelewa kutoka kwa vikundi vya wakulima, vyama vya ushirika na mashirika yasiyo ya kiserikali au kupitia usaidizi kutoka kwa serikali kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali 2.** Mikopo ya biashara ya kilimo inayofadhiliwa na serikali, mafunzo ya biashara na programu za chanjo ya magonjwa ya mifugo ni ya kawaida sana pamoja na programu zinazotoa vidole na malisho kwa wafugaji mbalimbali wa samaki.

**Jedwali 2**

Orodha ya vikundi vya wakulima, vyama vya ushirika, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo hutoa msaada wa aina mbalimbali kwa wakulima wa Kenya.

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Vikundi vya Kilimo | "Jitegemee Women's Group", "Muzulia Watane S. H. G.", "Chofumbo Agro-Ventures", "Imbinga S. H. G.", "Nyumba Kumi Initiative for Animal Anti-Theft", "Raa Women's Group", "Weshula Farmers' Group", "Furaha Initiative", "Mukangu Farmers' Society", "Dellosa Sunfields F. C. S. Ltd.", "Sabatia Micro & Small Enterprise Association" na "Shinyalu Poultry Entrepreneurship Group". |
| 2 | Vyama vya Ushirika | "Sabatia Dairy Co-operative Society", "Muvishi Dairy Co-operative Society", "Catholic Friend & Pentecostal Support", "Murhanda Co-operative Society", "Hamisi Co-operative Society" na "South Kabras Dairy Co-operative Society" |
| 3 | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | "Harvest of Hope", "Goldifarm Funds", "Sweet Potato Establishment & Feeds", "Community Health Volunteer Group (Vegetable Seed Distributors)", "Mainyoito Pastoralists Integrated Development Organisation (MPIDO)" na "One Acre Fund". |
| 4 | Serikali | "Cash Transfer for Orphans and Vulnerable Children (CT-OVC) Initiative", "Uwezo Fund", County Government "One Cow Initiative", "Poultry Subsidy Programme" na "Kenya Climate Smart Agriculture Project" (KCSAP). |

## HITIMISHO

Hitimisho lililofanywa katika utafiti huu lilizingatia maoni ya wafanyikazi wa mstari wa mbele katika mada ya ustawi wa wanyama kwa hiyo kuonyesha mitazamo ya ndani na nje. Hati hii imeonyesha kuwa viwango na desturi za ustawi wa wanyama huathiriwa zaidi na tamaduni, desturi, ushirikishwaji wa jamii, nguvu za kiuchumi na pengine ufahamu wa utunzaji wa wanyama kwa kiwango cha kawaida. Matokeo yanaonyesha wazi kwamba kunapaswa kuwa na uboreshaji katika utunzaji na ufugaji wa wanyama ambao unaweza kupatikana tu kwa kuchangia katika kuelimisha jamii zaidi kuhusu ustawi wa wanyama. Hapa, tunaona kuwa ujuzi wa ustawi wa wanyama unafanywa kuwa changamano tu kwa sababu ya ukosefu wa taarifa inayosababisha kuelewa duni kuhusu hii mada kwa wahusika. Hasa wafanyikazi wa mstari wa mbele na wakulima ambao hawataelewa lugha ya sheria kutoka kwa hati ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

machapisho ya serikali. Ni dhahiri kwamba ushiriki wa serikali ni mdogo na hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Mogoa na wenzake (2005) walioonyesha kuwa kuna ukosefu wa ufuatiliaji wa matukio ya ukatili wa wanyama, kusita kutekeleza sheria na kutofuata programu za mafunzo na uhamasishaji ili kuelimisha jamii juu ya masuala yanayohusu ustawi wa wanyama.

Hati hii imeangazia masuala makuu ya ustawi wa wanyama nchini Kenya na ni matumaini yetu kuwa wafanyikazi wa mstari wa mbele watajifunza kuwa macho katika masuala haya. Pia imefanya muhtasari wa sheria na kile ambacho wakulima na wafanyikazi wengine wanapaswa kujua na kuelewa kwa lugha rahisi na hivyo kuwaelimisha kuwa raia bora wa kutii sheria vilivyo. Kando na hiyo, imetaja vikundi mbalimbali vya kujisaidia na vyama vya ushirika ambavyo wakulima wanaweza kujiunga au kukaribia na wafadhili wanaweza kushirikiana navyo ili kutoa ufadhili wa shughuli za kilimo ambazo zinaweza kuleta matokeo mazuri. Ni faida kubwa kwa wafanyikazi wa mstari wa mbele kwamba makala haya pia yanataja vyanzo mbalimbali vya ufadhili ambavyo wanaweza kuangalia ikiwa kuna vikwazo vya kifedha.

Kudumisha ustawi wa wanyama kunahakikisha maisha ya wakulima na wadau wengine. Tunatumai kwamba uchapishaji wa matokeo haya utaanzisha mazungumzo kutoka kwa mtazamo wa ndani na kimataifa kuhusu kiwango cha ushiriki wa wafanyikazi wa mstari wa mbele kutoa mwanga zaidi katika ushiriki wao na nini kinaweza kuboreshwa. Kazi hii ilitoa fursa adimu ya kuingia uwanjani na kuhamasisha jamii mbalimbali juu ya umuhimu wa ustawi wa wanyama na kujenga umakini wa hali ya juu linapokuja suala la kugundua na kushuhudia unyanyasaji wa wanyama. Tunatumai matokeo haya yataadhiri sera za serikali kuhusu ustawi wa wanyama nchini Kenya kwa kutoa mapendekezo kutoka kwa mtazamo wa sahihi unaohakikisha kuanzishwa kwa mbinu mpya endelevu zinazoruhusu wakulima kufanya kazi pamoja na mashirika ya serikali kufuatilia utunzaji wa wanyama, afya na hali ya maisha kwa ujumla hivyo kuboresha ustawi wa wanyama.

## MAPENDEKEZO

### Suluhu za Kiutendaji na Mtazamo wa Baadaye

Katika siku zijazo, kazi itakayofanywa kwa hii mada inapaswa kuzingatia ustawi wa wanyama katika mikoa mingine ambayo haikujumuishwa katika utafiti huu na pengine kujumuisha wanyama wanaotumiwa kisayansi na wanyama pori pia. Hii itahakikisha kua matokeo ya kina ambayo yataathiri uundaji wa sera zinazohimiza matumizi ya kanuni za 3Rs (Burch na Russel, 1959) hata kuchangia zaidi katika juhudi za kupambana na ujangili.

Zaidi ya hayo, mipango ya kina inayolenga wakulima na wafanyikazi wengine wasio wa kitaaluma walio mstari wa mbele katika sekta ya kilimo inapaswa kutekelezwa ili kukuza uelewa wa kina wa kanuni za serikali kuhusu ustawi wa wanyama.

Mipango pia inapaswa kuanzishwa ili kushawishi uundaji wa sera dhabiti zinazoendeleza ustawi wa wanyama na kuondoa ukatili wa wanyama kupitia ushiriki wa mtetezi wa watunga sera husika ambao wako katika nyadhifa muhimu ili kuendeleza mabadiliko yanayohitajika.

### Mahali pa Kuripoti matukio au Kesi Zinazoshukiwa za Ukatili wa Wanyama

Sheria ya Katiba ya Kenya iliyotajwa hapo awali Nambari: CAP 360 Sehemu ya II Kifungu cha 30 kinasema kwamba wafanyikazi wa mstari wa mbele na wanajamii wengine wanaweza kuripoti masuala yanayohusu ukatili/unyanyasaji wa wanyama kwa polisi, chifu au viongozi wengine walioidhinishwa katika jamii.

Mbali na hayo, Chama cha Kenya cha Ulinzi na Kutunza Wanyama (*Kenya Society for the Protection & Care of Animals* - *KSPCA*) kimetoa taarifa zao za mawasiliano yaani barua pepe info@kspca-kenya.org na nambari za simu 0202430318, 0798303940 au 0733571125 kuripoti washukiwa. KSPCA ina ofisi na wawakilishi katika miji mikuu yote nchini Kenya.

## SHUKRANI

Mwandishi angependa kushukuru washiriki wote waliokubali kuhojiwa kwa ajili ya utafiti huu na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

wafanyikazi wenzake wa idara ya bakteria katika *Kenya Agricultural & Livestock Research Organisation* (KALRO) haswa Dkt. Monicah Maichomo, Dkt. Hezron Wesonga, Dkt. Moses Olum, Dkt. Nginyi, Dkt. Ascah Jesang, Eunice Ogugo, Gideon Ruto, Richard Keshura, Collins Mwenda, Edna Masila, Nathan Lagat na Janet Koros. Ufadhili wa kuandika hati hii ulitolewa na *Tiny Beam Fund, Inc*. (https://tinybeamfund.org).

## KAULI YA KIMAADILI

Makala haya ni tafsiri ua hati ya Memo ya Mwongozo iliyoandikwa kwa ajili ya *Tiny Beam Fund, Inc*. Ufafanuzi huu unakusudiwa kufikia hadhira kubwa zaidi na inalengwa kwa wazungumzaji wa Kiswahili ambao ni wafanyikazi wa mstari wa mbele linapohusu suala la utunzaji wa wanyama wa ustawi kwa jumla. Hakuna mgongano wa maslahi uliotangazwa. Taarifa zote na ushauri ni za mwandishi pekee.

## MAREJELEO

Alarcon, P., Fèvre, E. M., Muinde, P., Murungi, M. K., Kiambi, S., Akoko, J., & Rushton, J. (2017). Urban livestock keeping in the city of Nairobi: diversity of production systems, supply chains, and their disease management and risks. *Frontiers in Veterinary Science*, *4*, 171.

Broom, D. (1991). Animal Welfare: Concepts and Measurements. *Journal of Animal Science*, 69(10), 4167-4175.

Edwards-Callaway, L. N. & Calvo-Lorenzo, M. S. (2020). Animal Welfare in the US slaughter industry - a focus on fed cattle. *Journal of Animal Science*, *98*(4).

Greger, M. & Koneswaran, G. (2010). The public health impacts of concentrated animal feeding operations on local communities. *Fam Community Health, 33*(1), 373-382.

Greger, M. (2007). The long haul: risks associated with livestock transport. *Biosecurity and bioterrorism: biodefense strategy, practice, and science*, *5*(4), 301-312. doi: 10.1089/bsp.2007.0028

Greger, M. (2011). Transgenesis in animal agriculture and zoonotic disease resistance. *CAB Reviews: Perspectives in Agriculture, Veterinary Science, Nutrition & Natural Resources*, *6*(41).

Kimwele, C., Matheka, D., & Ferdowsian, H. (2011). A Kenyan perspective on the use of animals in science education and scientific research in Africa and prospects for improvement. *Pan African Medical Journal*, *9*(1).

Manning, J., Power, D., & Cosby, A. (2021). Legal Complexities of Animal Welfare in Australia: Do On-Animal Sensors Offer a Future Option?. *Animals*, *11*(1), 91.

Mogoa, E. G., Wabacha, J. K., Mbithi, P. M., & Kiama, S. G. (2005). An overview of animal welfare issues in Kenya. *Kenya Veterinarian*, *29*, 48-52.

Molomo, M., & Mumba, T. (2014). Drivers for animal welfare policies in Africa. *Revue Scientifique et Technique (International Office of Epizootics)*, *33*(1), 47-53.

Njisane, Y. Z., Mukumbo, F. E., & Muchenje, V. (2020). An outlook on livestock welfare conditions in African communities—A review. *Asian-Australasian Journal of Animal Sciences*, *33*(6), 867-878.

OIE – Terrestrial Animal Health Code. (2019). *Section 7: Animal Welfare, Chapter 7.1: Introduction to the recommendations for animal welfare", 7.1.1-7.1.5*

Rioja-Lang, F.C., *et al*. (2020). Prioritization of Farm Animal Welfare Issues Using Expert Consensus. *Frontiers in Veterinary Science*, *6*(495).

Russel, W., & Burch, R. (1959). The Principles of Humane Experimental Technique; as reprinted 1992. *Universities Federation for Animal Welfare: Wheathampstead, UK*.

Thornton, P. K. (2010). Livestock production: recent trends, future prospects. *Philosophical Transactions of the Royal Society B: Biological Sciences*, *365*(1554), 2853-2867.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.626

Thumbi, S. M., Njenga, M. K., Marsh, T. L., Noh, S., Otiang, E., Munyua, P., ... & McElwain, T. F. (2015). Linking human health and livestock health: a "one-health" platform for integrated analysis of human health, livestock health, and economic welfare in livestock dependent communities. *PloS one*, *10*(3), e0120761.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.